# CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM
## TAASISI YA TAALUMA ZA KISWAHILI

# UFADHILI WA MASOMO YA M.A. KISWAHILI

Taasisi ya Taaluma za Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, (UDSM) kwa kushirikiana na Kampuni ya ALAF Limited, inapenda kutangaza ufadhili wa ada kwa wanafunzi watatu (3) waliochaguliwa kusoma Programu ya M.A. Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa mwaka wa masomo 2025/2026.

### Sifa za Mwombaji

1. Awe raia wa Tanzania.
2. Awe mhitimu wa Shahada ya Awali katika Kiswahili au programu husiani na kufaulu vizuri kozi za Kiswahili. Kipaumbele kitatolewa kwa wahitimu wa Shahada ya Awali katika Kiswahili.
3. Awe na WAKIA (GPA) usiopungua 3.8 wa digrii ya kwanza.
4. Awe amepata au ameomba udahili katika Programu ya Shahada ya Umahiri katika Kiswahili ya UDSM.
5. Awe na umri usiozidi miaka 25 wakati analeta maombi.
6. Awe mhitaji wa ufadhili wa ada.
7. Awe na uwezo wa kujigharimia mahitaji mengine (chakula, steshenari, malazi, utafiti n.k.).

### Nyaraka Zinazohitajika

1. Nakala ya cheti cha matokeo ya kitaaluma ya shahada ya kwanza (Transcript)
2. Nakala ya cheti cha kuzaliwa
3. Maelezo mafupi (ukurasa mmoja) yanayobainisha sababu za kuhitaji ufadhili wa ada

### Maombi yatumwe kwa:

Mkurugenzi,
Taasisi ya Taaluma za Kiswahili.
Baruapepe: iks@udsm.ac.tz

**Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 07/12/2025 Saa sita usiku.**